



Kuamini mikosi ni shirki, Kuamini mikosi ni shirki, Kuamini mikosi ni shirki, alisema hivyo mara tatu", Na hakuna yeyote miongoni mwetu isipokuwa ana chembe ya hilo, isipokuwa Mwenyezi Mungu huliondoa kwa kumtegemea

Kutoka kwa Abdallah bin Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -
Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Kuamini mikosi ni shirki, Kuamini mikosi ni
shirki, Kuamini mikosi ni shirki, alisema hivyo mara tatu", Na hakuna yeyote miongoni
mwetu isipokuwa ana chembe ya hilo, isipokuwa Mwenyezi Mungu huliondoa kwa
kumtegemea.

[Sahihi] [Imepokelewa na Abu Daud, Tirmidhiy, Ibn Majah na Ahmad]

Ametahadharisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kutokana na imani ya mikosi:
Nayo ni kuamini mikosi ya chochote chenye kusikika au chenye kuonekana, kama ndege au
wanyama au walemavu au namba au siku au kinginecho, Na bila shaka ametaja ndege kwa
sababu ndio ilikuwa maarufu kipindi cha zama za ujinga, na asili yake ni kumuachia ndege
aruke katika jambo kama safari au biashara au kinginecho, akiruka pande wa kulia anajipa
bishara na anatekeleza anachotaka kukifanya, na akirukia upande wa kushoto, anaamini ni
mkosi na anaacha kufanya alichotaka kukifanya. Na akaeleza kuwa kitendo hicho ni
ushirikina, na mikosi imekuwa ni ushirikina kwa sababu hakuna aletaye kheri ila Mwenyezi
Mungu, na wala hazui shari ila Mwenyezi Mungu yeye pekee asiye na mshirika. Na ametaja
bin Masoud radhi za Allah ziwe juu yake kuwa inaweza kuingia katika moyo wa muislamu
kiasi kidogo cha imani ya mkosi, lakini anatakiwa akizuie kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu,
ikiwa ni pamoja na kufanya sababu.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3383>

